



---

**TRANSLATION**  
**FOREIGN POLICY EXCERPTS U.S. PRESIDENT BARACK OBAMA**  
**ADDRESS TO JOINT SESSION OF CONGRESS**  
**TUESDAY, FEBRUARY 24TH, 2009**

Mpango wa kupata nafuu na mpango wa uthabiti wa kifedha ni hatua za haraka tunazochukua kufufua uchumi wetu mnamo muda mfupi. Lakini njia ya pekee ya kurejesha nguvu za uchumi wa Marekani ni kufanya uwekezaji wa muda mrefu ambao unazalisha nafasi mpya za kazi, viwanda vipya na uwezo mpya wa kushindana na mataifa mengine duniani. Njia ya pekee ambayo karne hii itakuwa karne nyingine ya Kimarekani ni kama mwishowe tutakabili gharama za utegemeaji wetu wa mafuta na gharama kubwa za huduma za afya; shule ambazo haziwatayarishi watoto wetu na mlundikano wa madeni ambayo huenda watarithi. Huo ni wajibu wetu."

"Katika bajeti hii, tutakomesha mipango ya elimu ambayo haifanyi kazi na kukomesha malipo ya moja kwa moja kwa mashirika ya biashara ya kilimo ambayo hayahitaji malipo hayo. Tutatokomeza mikataba isiyoabuniwa ambayo imepoteza mabilioni ya fedha nchini Iraq, na kurekebisha bajeti yetu ya ulinzi ili tusiwe tunalipia mifumo ya silaha ya enzi za Vita baridi ambayo hatuitumii. Tutateketeza ubadhirifu, wizi na matumizi mabaya katika mipango yetu ya huduma za afya ambayo haiwawezeshi wazee wetu kuwa na afya bora na tutarejesha hisi ya haki na usawa katika kode ya ushuru kwa hatimaye kukomesha nafuu ya kodi inayotolewa kwa mashirika ya biashara ambayo yanahamishia kazi zetu ng'ambo.